

KUNAWA MIKONO KWA MAJI SAFI NA SABUNI IWE NI TABIA

Na Abdallah Mahia (12 Juni, 2022)

Usafi ni jambo muhimu sana katika suala la afya ya jamii yenye kupunguza maambukizi na athari za maradhi.

Kupungua haraka kwa vifo vinavyotokana na magonjwa ya kuambukiza kulikoonekana katika nchi tajiri mnamo karne iliyopita kusingeweza kufikiwa bila uboreshaji na uhamasishaji unawaji mikono wa hali ya juu kwa afya ya jamii na kuwezesha watu kujali zaidi usafi pale ambapo maji safi yaliwafikia majumbani mwao, na bei ya sabuni ilipokuwa nafuu kiasi kwamba ilikuwa rahisi kuweka sabuni katika kila sinki.

Hatimaye juhudi za pamoja baina ya harakati za wataalam wa afya ya jamii na sekta binafsi zimwezesha mambo kama vile usafi wa mikono, makazi, na katika maisha kuwa ni sehemu ya maisha ya jamii. Kwa bahati mbaya, katika nchi maskini habari hizi hazijaleta tofauti ya maisha.

Nakumbuka katika nchi hizi masikini hadi kufikia mwishoni mwa karne ya 20, watu bilioni mbili bado hawakuwa na uwezo wa kupata maji safi na salama kadiri inavyotakiwa, na watu bilioni moja hawakuwa na maji safi ya kunywa yanayotosheleza mahitaji yao. Jitihada za kuhamasisha kwa ufanisi hali ya usafi zimekuwa zikienda polepole sana na mara nyingi bila mafanikio.

Ingawa maendeleo ya viwanda kwa nchi zilizoendelea yamerahisisha upatikanaji wa sabuni majumbani, bado haijafanikiwa kuhamasisha hali ya usafi au mwamko wa watu kuhusu unawaji mikono kwa sabuni kwa kiwango cha juu ili kwenda sambamba na matokeo ya maendeleo hayo.

Hii ni fursa adimu kwa afya ya jamii kama ilivyoelezwa awali. Vyanzo vikuu viwili vya vifo vya watoto katika nchi zinazoendelea kwa sasa ni magonjwa ya kuhara na maambukizi ya mfumo wa upumuaji hivyo kitendo kidogo tu cha kunawa mikono kwa maji safi na sabuni kinaweza kuondoa takribani nusu ya hatari ya kuambukizwa magonjwa ya kuhara na takribani theluthi ya maambukizi ya mfumo wa upumuaji. Hali hii inakifanya kitendo cha kunawa mikono kuwa



chaguo bora zaidi la kuzuia maambukizi ya magonjwa kuliko chanjo au kinga nyingine yoyote.

Ikiwa nchi zinazoendelea zinataka kufikia hali hiyo ya kupunguza vifo vya watoto ambapo ajenda hii iliyosahaulika katika karne ya 20 haina budi kutiliwa maanani sasa na haitoshi tu maji safi na salama kupatikana kote, bali pia tabia ya kunawa mikono kwa maji safi na sabuni lazima iwe kwa watu wote. Jambo hili linahitaji ushirikiano kati ya Wizara za Afya, wizara ya Elimu na ufundi stadi, wizara ya Maji pamoja na asasi zisizo za serikali na jumuiya za kijamii kutumia kila fursa iliyopo kuinua mwamko wa watu kuhusu unawaji mikono kwa maji safi, salama na sabuni.

Aidha, sekta binafsi, ambazo zilichangia kwa kiasi kikubwa kupandisha viwango vya hali ya usafi katika nchi tajiri, zinaweza kufanya vivyo hivyo pale inapopanua shughuli zake katika nchi zinazoendelea.

Jambo la Kunawa mikono kwa maji safi na sabuni lazima liwe jambo la kawaida katika nchi zinazoendelea. Ili jambo hili liweze kufanyika ni lazima kuhakikisha kila mmoja anafahamu umuhimu wa kunawa mikono kwa maji safi na sabuni, kuanzisha ushirikiano baina ya sekta ya umma (serikali) na binafsi (wadau), kuandaa wataalam na raslimali zinazotakiwa katika kufanikisha unawaji wa mikono, kutumia mawasiliano ya hali ya juu yatakayowezesha watu wengi kadiri iwezekanavyo kupata taarifa ili kuhamasisha unawaji mikono kwa maji safi salama na sabuni, kuonesha kwamba mabadiliko ya tabia yanayopimika yanaweza kufikiwa kwa kupitia gharama nafuu.

Naipongeza serikali kwa jitihada zake zinaonekana kupitia wizara ya Afya chini ya kampeni ya Kitaifa ya Afya na usafi wa Mazingira kwa jamii ya watanzania kuanza kujua umuhimu wa unawaji wa mikono kwa maji safi salama na sabuni kwa kiwango cha wastani na hivyo basi kilichobakia ni kuendelea kuzidisha jitihada kwa watanzania na kuhakikisha kasi ya kuongeza huduma ya maji safi kila kona ya nchi kupitia wizara ya maji pamoja na wadau mbalimbali inaendelea, hii itaifanya serikali na jamii ya watanzania kufikia lengo lililokusudiwa.

Tutambue kuwa suala la usafi wa kunawa mikono huenda sambamba na upatikanaji wa maji safi na salama kwa kila sehemu.

Katika ulimwengu tulionao wenye pilika nyingi zinazotokana na ushindani wa kutafuta mbinu na njia tofautitofauti za kutuma ujumbe kuelekea kwa watu kutoka pande zote za dunia ili jamii ielimike inahitaji kampeni madhubuti tu na zilizobuniwa vizuri ndizo zinaweza kuleta mabadiliko ya tabia.

Kwa nchi kama Tanzania tumethubutu, kilichobakia ni kuzidi kuweka hamasa na Elimu zaidi kwa jamii na kufanya tendo la **kunawa mikono kwa maji safi salama na sabuni iwe ni kawaida na tabia ya kila mtu.**

"Hakuna lisilowezekana"

Abdallah Mahia ni Afisa Afya wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma.